JINSI YA KUWASAIDIA

# MANUSURA NA WAHANGA WA UNYANYASAJI

## Wa Kijinsia Pale Mtetezi Wa Kampeni Dhidi Ya GBV (Ukatili wa Kijinsia) Hayupo Katika Eneo Lako



Kitabu cha Mwongozo cha hatua kwa hatua kwa watendaji katika masuala ya maendeleo na utu nchini Tanzania

UNITED NATIONS TANZANIA
UN WOMEN
UNFPA
unicef for every child

Toleo hili la Kitabu cha Mwongozo wa Unyanyasaji wa Kijinsia lilitolewa mwaka 2023 kwa msaada wa Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN RCO), Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF), Shirika la Wanawake la Umoja wa Mataifa (UN Women), Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) Tanzania. Linatokana na rasilimali za uwakala zilizoidhinishwa baina ya mataifa na zimetoholewa katika mkutadha wa Tanzania. Kutohoa na kutafsiri kwa Kitabu cha Mwongozo kuliongozwa na Mtandao wa Ulinzi Dhidi ya Unyanyasaji na Ukatili wa Kingono (PSEA) Tanzania na msaada wa ziada wa kiufundi kutoka kwa wataalamu wa ukatili wa kijinsia (GBV) na ukatili dhidi ya watoto (VAC). Taarifa ya nyongeza katika muktadha wa Tanzania, rasilimali za rufaa na istilahi ya mahali vilikuwa vitu muhimu vilivyotoholewa.

Toleo la Mwongozo huu linapatikana kwa lugha za Kiingereza na Kiswahili.

# Je, *Kitabu cha Mwongozo* ni nini?

Kitabu cha Mwongozo na nyenzo[1] zake hutoa maelezo kwa **watendaji wote wa masuala ya kibinadamu/kiutu Tanzania** kuhusu:

- Jinsi ya kumsaidia manusura/mhanga wa unyanyasaji wa kijinsia (GBV) au unyanyasaji na ukatili wa kingono (SEA)
- Wanaokwambia uzoefu wao wa matukio ya GBV au SEA
- Katika mkutadha ambao hakuna mtetezi wa kampeni dhidi ya GBV (kwa kujumuisha njia za rufaa au wapokea taarifa za PSEA) anayepatikana.

*Kitabu cha Mwongozo* hutumia viwango vya kiulimwengu katika kutoa msaada wa msingi na habari kwa manusura wa GBV na SEA bila kusababisha madhara zaidi. Wakati Kitabu cha Mwongozo kinatumia mfumo wa Huduma ya Kwanza ya Kisaikolojia (PFA) (Andaa, Angalia, Sikiliza na Unganisha), elimu au mafunzo ya zamani juu ya PFA hayahitajiki. *Mafunzo ya kina ya PFA yanahimizwa.*



[1] Kuandamana na Kijitabu cha Mwongozo ni Dokezo la Historia na Vidokezo kwa Mtumiaji/Jinsi ya Kuongoza.

# Tafsiri Muhimu

## Unyanyasaji wa kijinsia (GBV)

GBV ni istilahi inayohusisha kitendo chochote chenye madhara kinachotendwa dhidi ya mtu kwa msingi wa tofauti za kijamii kati ya wanaume na wanawake (jinsia). Inajumuisha vitendo vinavyomuumiza mtu kimwili, kimapenzi, kiakili, vitisho vya vitendo hivyo, vya kumlazimisha mtu, na vitendo vingine vinavyonyima uhuru.

## Unyanyasaji wa Kijinsia kwa Watoto

Kitendo chochote cha kujamiiana kati ya mtoto na mtu mzima/mtoto mkubwa. Kinahusisha ama matumizi ya nguvu au kulazimisha, au katika mazingira ambapo ridhaa ya mhanga inakosekana kwa sababu ya umri wake mdogo.

## Unyanyasaji na Ukatili wa Kingono (SEA)

hutokea iwapo watu wenye mamlaka au nafasi ya kuaminiwa kutoka kwa jumuiya ya kimaendeleo na masuala ya kibinadamu (kama vile Umoja wa Mataifa, mashirika yasiyo ya kiserikali, na wabia) wanatumia hali ya wanaoweza kudhuriwa wa jumuiya zilizoathiriwa kwa madhumuni ya unyanyasaji wa kijinsia. Ni muhimu kukumbuka kwamba ridhaa haiwezi kuamua kama unyanyasaji wa kijinsia umetokea kwa vile wahanga wana hali ya uwezo usiolingana.

## GBV dhidi ya SEA

SEA ni aina mojawapo ya GBV, kwa vile wahanga wa SEA mara nyingi wananyanyaswa kwa sababu ya kutolindwa, hadhi ya mkingamano kama wanawake, wasichana, wavulana, au hata wanaume (katika baadhi ya mazingira). Ni amri kwa utoaji wa taarifa za SEA kwamba unawakilisha tofauti muhimu kati yake (kama GBV hauna amri kwa utoaji wa taarifa).

## Mhanga/manusura

Ni mtu ambaye amefanyiwa ukatili wa kijinsia au kujaribu kufanyiwa ukatili wa kijinsia. Istilahi zote mbili zinaweza kutumika kwa kubadilishana.

# Yaliyomo


| Sehemu | Ukurasa | Tumia kwa |
|---|---|---|
| Ujumbe muhimu | 6 to 8 | Mwongozo wa haraka |
| Mti wa uamuzi | 10 & 11 | |
| Karatasi ya Maelezo kuhusu huduma zinazopatikana | 13 to 15 | |
| Mambo ya Kufanywa, ya Kutofanywa na ya kusema | 17 | |
| Angalia | 17 | |
| Sikiliza | 18 & 19 | |
| Unganisha | 19 & 20 | |
| Mwongozo wa hatua kwa hatua | 22 | Maandalizi na kupata elimu na maarifa na ujuzi wa kushughulikia jambo fulani |
| Mtazamo Wa Manusura/Mhanga | 22 | |
| Unyanyasaji Na Ukatili Wa Kingono | 23 to 25 | |
| Jiandae, Angalia, Sikiliza & Unganisha | 26 to 30 | |
| Watoto na vijana (kuanzia kubalehe hadi miaka 18) | 32 | Mwongozo wa haraka kwa watoto na vijana chini ya miaka 18 |
| Ujumbe muhimu | 32 | |
| Ikiwa mtu anakuuliza msaada kumhusu mtoto/kijana aliye na hitaji… | 34 | |
| Ikiwa mtoto/kijana anakuomba msaada | 34 to 36 | |
| Marejeo kwa umri na uwezo wa watoto kufanya maamuzi | 37 | |

# Ujumbe Muhimu

**Siku zote zungumza na mtaalamu wa GBV kwanza** ili kufahamu ni huduma na msaada upi wa GBV zinapatikana katika eneo lako. Baadhi ya huduma zinaweza kupatikana kwa njia ya huduma ya mawasiliano ya simu ya moja kwa moja, dawati la huduma ya msaada, na/au mitindo mingine ya msaada mwingine toka mbali.


**Fahamu huduma nyingine zozote zinazopatikana** katika eneo lako. Tambua huduma zitolewazo na wabia wa maendeleo na masuala ya kibinadamu kama vile afya, msaada wa kisaikolojia, mahali pa kujisitiri na bidhaa zisizo za chakula. Zingatia huduma zinazotolewa na jamii kama vile misikiti/makanisa, vikundi vya kina mama na mashirika yanayotoa huduma za walemavu.

**Kumbuka wajibu wako.** Sikiliza bila kuhukumu. Toa habari zilizo sahihi, mpya kabisa kuhusu huduma zinazopatikana. Mwache manusura/mhanga aamue mwenyewe. Fahamu mambo unayoweza na usiyoweza kuyasimamia. Hata bila ya kuwa na mtetezi wa kampeni dhidi ya GBV katika eneo lako, kunaweza kuwa na wabia wengine, kama vile ulinzi wa mtoto au mtaalamu wa afya ya akili, ambaye anaweza kuwasaidia manusura/wahanga wanaohitaji uangalizi na msaada wa ziada. Omba idhini ya manusura/mhanga kabla ya kuwaunganisha kwa mtu yeyote. Usimlazimishe manusura/mhanga iwapo anasema hapana.

Usiwatambue au kuwatafuta manusura/wahanga wa GBV. Patikana ikiwa mtu anaomba msaada.

**Kumbuka udhamini wako.** Watendaji wote wa maendeleo na masuala ya kibinadamu wamedhaminiwa kutoa msaada bila ya kuhukumu na kuwabagua watu wenye uhitaji bila ya kujali sura ya mtu, hali ya ndoa, hali ya ulemavu, umri, kabila/mbari/dini, nani alisababisha, alifanya unyanyasaji, na katika hali ambayo unyanyasaji ulifanywa.

Tumia **njia inayomlenga manusura/mhanga** kwa kuwa na:



**Ikiwa huduma za afya zipo, siku zote toa habari juu ya kinachopatikana.** Shirikisha unachokifahamu, na muhimu sana elezea usichokifahamu. Mwache manusura/mhanga aamue ikiwa anataka kuzipata. Kupata huduma bora za matibabu ndani ya saa 72 kunaweza kuzuia maambukizo ya kingono (STIs), na ndani ya saa 120 kunaweza kuzuia mimba isiyohitajika.


Toa nafasi kwa watu walio na ulemavu kuwasiliana nawe bila ya kuwepo kwa mwangalizi wao, ikiwa wanapendelea hivyo (na hakuhatarishi au kusababisha mvutano katika uhusiano huo).

Unyanyasaji wa kijinsia asili yake ni matumizi mabaya ya madaraka, matumizi ya nguvu, na kaida zenye madhara, na wachache fulani mara nyingi wana hatari zaidi ya madhara na unyanyasaji kwa sababu ya hali zao binafsi. Kwa mfano, kama mwanaume au mvulana akinyanyaswa, hakubadilishi utambulisho wake.

**Kwa hiyo, ni muhimu kusikiliza kwa umakini na kujitahidi kuwasaidia manusura/wahanga wote, wanawake, wanaume, wavulana, na wasichana, bila ya kuwabagua.**

Yeyote anaweza kufanya kitendo cha unyanyasaji wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na mume/mke, mwenzi, mwanafamilia, mwangalizi, mkwe/shemeji/wifi, mgeni, mzazi, au yeyote anayebadilishana fedha au vitu kwa kitendo kwa ngono.

Yeyote anaweza kuwa manusura/mhanga wa unyanyasaji wa kijinsia – hii ni pamoja na, lakini si tu watu waliooana, wazee au watu wanaojishughulisha na kazi ya ngono.



## Mifano ya Wahalifu wa GBV

- Mwenzi/Mpenzi
- Mtu wa karibu, i.e., Mume, mke, mpenzi
- Mwanafamilia
- Mkwe
- Mtu usiyemfahamu/mgeni
- Mzazi/Mlezi
- Mtu ambaye hubadilishana pesa au bidhaa kwa ajili ya tendo la ngono



## Mifano ya walionusurika/waathirika wa GBV

- Watu waliolewa
- Wazee
- Watu wanaojishughulisha na biashara ya ngono

**Linda utambulisho na usalama wa manusura/mhanga. Usiandike, usipige picha, au kutoa habari/utambulisho wowote binafsi unaomuhusu manusura/ mhanga au uzoefu wao, ikiwa ni pamoja na msimamizi wako. Weka simu na kompyuta mbali kuepuka wasiwasi kwamba sauti ya manusura/mhanga inarekodiwa.**

- Habari/utambulisho binafsi ni pamoja na jina la manusura/mhanga, jina la mnyanyasaji, tarehe ya kuzaliwa, namba ya usajili, anwani ya nyumbani, anwani ya kazini, mahali watoto wao wanaenda shuleni, muda na mahali sahihi tukio lilipotokea n.k.
- Shirikisha habari ya jumla, isiyomtambulisha mtu.
  - Kwa timu au wabia wa sekta yako katika jitihada za kufanya mpango wako kuwa salama zaidi.
  - Kwa mtandao wako wa msaada wakati ukitafuta utunzaji binafsi na kutiwa moyo.

## Mifano ya jinsi ya kushirikisha kwa usalama hatari na mwelekeo uliobainishwa:

*"Nimefahamu ya kwamba watu wanasumbuliwa karibu na eneo la maji kwa sababu limejitenga na lipo mbali. Tunaweza kujaribu kupunguza usumbufu huu kwa kuhimiza utumiaji wa eneo la maji lililo karibu, au kuhimiza kuchota maji katika vikundi, au…"*

*"Mtu fulani alinishirikisha jambo fulani baya lililowatokea. Siwezi kushirikisha kila kitu, lakini nahitaji msaada kuhusiana na jinsi mwingiliano huu unavyoniathiri."*

# Ninatakiwa kufanya nini endapo muhanga wa ukatili wa kijinsia akinifuata?

# Mti wa Uamuzi



## ANDAA

**Angalia huduma zilizopo.**



## Tukio la GBV linafunuliwa kwako...

### Na mtu mwingine...

Toa habari mpya kabisa na sahihikuhusu huduma zozote na msaada unaoweza kupatikana kwa manusura/mhanga. Mhimize mtu binafsi kushirikisha habari hii kwa usalama na kwa usiri kwa manusura/mhanga ili waweze kueleza wanavyopenda. ANGALIA: USIWATAFUTE manusura/wahanga wa GBV.

**ANGALIA:** USIWATAFUTE manusura/wahanga wa GBV.

### Ndiyo


Toa habari za kina kuhusu rasilimali/huduma zipatikanazo ikiwa ni pamoja na jinsi ya kuzifikia, saa na maeneo yanayofaa, watoa taarifa za PSEA kwenye huduma, uchaguzi wa usafiri salama n.k. Usishirikishe habari kumhusu manusura/mhanga au jambo alilopitia kwa yeyote bila ya idhini yake. Usirekodi kila kitu cha tukio au vitu vya kumtambulisha manusura/mhanga kibinafsi.

**Na manusura/mhanga mwenyewe**

**ANGALIA & SIKILIZA**
*(rejea ukurasa wa 17 to 19)*

Jitambulishe. Uliza jinsi unavyoweza kusaidia. Weka heshima, usalama, usiri na kutobagua.

***Kwa watoto na vijana (kuanzia kubalehe hadi miaka 18), nenda kwenye ukurasa wa 16.***



**Je, mdau dhidi ya GBV/ njia ya rufaa inapatikana?**


**Ndiyo**

Fuata njia ya rufaa ya GBV kumfahamisha manusura/mhanga kuhusu huduma zipatikanazo za GBV na umpatie rufaa ikiwa unapewa idhini na manusura.

**Hapana**

**UNGANISHA**
*(rejea ukurasa wa 19 & 20)*

Toa habari sahihi kuhusu huduma zipatikanazo.



**Je, manusura/ mhanga amechagua kuunganishwa kwa huduma yoyote?**

**Hapana**


Dumisha usiri. Elezea kwamba manusura/mhanga anaweza kubadilisha mawazo yake na kutafuta huduma na baadaye. Ikiwa huduma ni za muda mfupi, za kusongezwa au zinapatikana kwa muda mfupi, toa habari ni lini huduma hizi zitakoma kupatikana.

**Ni huduma zipi za kimsaada zinazofaa ambazo ninaweza kumwambia muhanga kulingana na msaada anaohitaji?**

# Fomu Ya Taarifa

Jaza fomu hii ya taarifa kwa huduma katika eneo lako na uiweke sehemu ambayo inaweza kufikiwa kwa urahisi.

Fanya kazi na mtaalamu wa GBV, kiongozi wa timu yako na wabia kutambua:




## Ulinzi wa Mtoto

Taarifa:______________________________________________

Watu husika:__________________________________________

## Afya ya akili/msaada wa saikolojia ya jamii

Taarifa:______________________________________________

Watu husika:__________________________________________

## Afya

Taarifa:__________________________________________________________

Watu husika:______________________________________________________

## Afya ya kujamiana na uzazi

Taarifa:__________________________________________________________

Watu husika:______________________________________________________

## Bidhaa zisizo za chakula/SAFISHA ikiwa ni pamoja na vifaa vya hadhi

Taarifa:__________________________________________________________

Watu husika:______________________________________________________

## Mahali pa kujisitiri

Taarifa:__________________________________________________________

Watu husika:______________________________________________________

## Sheria

Taarifa:__________________________________________________________

Watu husika:______________________________________________________

## Chakula na lishe

Taarifa:__________________________________________________________

Watu husika:______________________________________________________

## Huduma kwa vijana waliobalehe hadi kufikia umri wa miaka 18/vijana

Taarifa:__________________________________________________________

Watu husika:______________________________________________________

## Huduma kwa watu wenye ulemavu

Taarifa:_______________________________________________________________________

Watu husika:___________________________________________________________________

## Huduma ya walengwa wengine wa kijinsia

Taarifa:_______________________________________________________________________

Watu husika:___________________________________________________________________

## Huduma kwa kaya zinazoongozwa na mtoto au mwanamke

Taarifa:_______________________________________________________________________

Watu husika:___________________________________________________________________

## Mtandao wa PSEA

Taarifa:_______________________________________________________________________

Watu husika:___________________________________________________________________

## Nyingine:

Taarifa:_______________________________________________________________________

Watu husika:___________________________________________________________________

## Nyingine:

Taarifa:_______________________________________________________________________

Watu husika:___________________________________________________________________


# Ninatakiwa kuwaje katika hali hii?

## Vitu muhimu vya “kufanya” na “kutofanya”?

# Mambo ya kufanya, kutofanya na nini cha kusema

*Kwa watoto na vijana (kuanzia kubalehe hadi kufikia miaka 18), nenda kwenye ukurasa wa 16.*

## ANGALIA



| Mambo Ya Kufanya | Mambo Ya Kutofanya |
| --- | --- |
| MRUHUSU manusura/mhanga kukaribia. Sikiliza mahitaji yao. | USIMPUUZE yeyote anayekukaribia na kukushirikisha kwamba amepitia jambo baya, jambo linalomkosesha raha, jambo baya na/au linalokasirisha. |
| MUULIZE jinsi unavyoweza kumsaidia kwa mahitaji ya msingi na ya dharura kwanza. Manusura/wahanga wengine wanaweza kuhitaji huduma ya matibabu mara moja au nguo. | USILAZIMISHE msaada kwa watu kwa kuwa mtu wa kuingilia au kusukumasukuma mambo. |
| MUULIZE manusura/mhanga iwapo anaona sawa kuzungumza nawe katika sehemu uliyoko sasa. Iwapo manusura/mhanga ameambatana na mtu fulani, usichukulie kwamba ni salama kuzungumza na manusura/mhanga kuhusu tukio lake mbele ya mtu huyo. | USIONYESHE hisia sana. Kuwa mtulivu. |
| TOA msaada wa kuonekana kama vile kumpa maji, sehemu ya faragha ya kukaa, karatasi shashi n.k. | USIMLAZIMISHE manusura/mhanga kukushirikisha habari zaidi kuliko zile anazoona raha kukushirikisha. Utondoti wa jambo lililotokea na lilimtokea nani si muhimu au kuhitajika kwa wajibu wako katika kusikiliza na kutoa habari juu ya huduma zinazopatikana. |
| FANYA, kwa kadri ya uwezo wako, kumuuliza manusura/mhanga kumchagua mtu anayefarijika naye kumtafsiria na/au kumsaidia iwapo inahitajika. | USIULIZE iwapo mtu amepitia GBV, amebakwa, amegongwa n.k. |

### Mifano ya mambo ya kusema…

- “Unaonekana kuwa na uchungu mwingi sasa, je, ungependa kwenda mahali pa ushauri wa kiganga au matibabu?”
- “Je, mahali hapa ni SAWA kwako? Je, kuna mahali pengine ambapo ungejisikia vizuri zaidi? Je, unafarijika kufanya mazungumzo hapa?”
- “Je, ungependa kupata maji? Tafadhali jisikie huru kukaa.”

## SIKILIZA

| Mambo Ya Kufanya | Mambo Ya Kutofanya |
|---|---|
| WEKA usiri kwenye habari yoyote uliyoshirikishwa. Iwapo unahitaji kutafuta ushauri au mwongozo jinsi ya kumsaidia manusura/mhanga vizuri zaidi, omba idhini yake kuzungumza na mtaalamu au mwenzako. Fanya hivyo bila ya kusema mambo binafsi yanayomtambulisha manusura/mhanga. | USIANDIKE chochote, usipige picha za manusura/mhanga, kurekodi mazungumzo kwenye simu yako au kwenye kifaa kingine, au kuwafahamisha wengine vikiwemo vyombo vya habari. |
| FANYA kudhibiti matarajio yoyote kuhusu vikwazo vya usiri wako, **ikiwa yanatumika katika mazingira yako.**[2] | |
| SIMAMIA matarajio ya wajibu wako. | USIULIZE maswali kuhusu jambo lililotokea. Badala yake, sikiliza na uliza unachoweza kufanya ili kusaidia. |
| SIKILIZA zaidi kuliko unavyozungumza. | USILINGANISHE uzoefu wa mtu na jambo lililotokea kwa mtu mwingine. Usiseme kwamba hali “si jambo kubwa” au muhimu. Jambo muhimu ni kwa jinsi gani manusura/mhanga anajisikia kuhusu jambo lililotokea kwake. |
| USISEME maneno ya faraja na msaada; sisitiza kwamba jambo lililotokea kwake halikuwa kosa lake. | USIWE na shaka au kupinga jambo analokuambia mtu. Kumbuka wajibu wako ni kusikiliza bila kuhukumu na kutoa habari kuhusu huduma zinazopatikana. |

[2] Kuna mazingira ambayo yana sheria za kutoa taarifa kwa lazima zinazohusiana na aina fulani ya kesi. Rejea kwa watoa taarifa za PSEA na/au mtaalamu wa GBV kwa maelezo zaidi na mwongozo.

## Mifano ya mambo ya kusema…

- “Ni jinsi gani naweza kukusaidia?”
- “Sitamshirikisha mtu habari bila idhini yako (mambo ya SEA)/idhini (mambo ya GBV).”
- “Nitajaribu kukusaidia kadri niwezavyo, lakini mimi siyo mshauri. Naweza kukushirikisha habari yoyote niliyo nayo juu ya msaada unaopatikana kwako.”
- “Tafadhali nishirikishe chochote unachotaka kunishirikisha. Huhitaji kunieleza kuhusu jambo lililokupata ili mimi nikuhabarishe juu ya msaada unaopatikana kwako.”
- “Nasikitika hili lilitokea kwako.”
- “Jambo lililotokea halikuwa kosa lako.”

# UNGANISHA

## Mambo Ya Kufanya

HESHIMU haki za manusura/mhanga kufanya uamuzi wake mwenyewe.

SHIRIKISHA habari juu ya huduma zote zinazopatikana, hata kama si huduma maalum za GBV.

MWAMBIE manusura/mhanga kwamba hahitaji kufanya uamuzi wowote sasa, yeye anaweza kubadilisha mawazo yake na kupata huduma hizi hapo baadaye.

ULIZA kama kuna mtu, rafiki, mwanafamilia, mtunzaji au yeyote ambaye manusura/mhanga anamwamini kwenda kutafuta msaada kwake.

## Mambo Ya Kutofanya

USITIE chumvi kwenye ujuzi wako, kutoa ahadi za uwongo au kutoa habari za uwongo.

USITOE ushauri au maoni yako mwenyewe juu ya hatua bora ya kuchukua au jambo la kufanya baadaye.

USICHUKULIE kwamba unafahamu jambo ambalo mtu mwingine anahitaji. Hatua zingine zinaweza kumweka mtu katika hatari zaidi ya kunyanyapaliwa, kulipiza kisasi, au madhara.

USICHUKULIE kwamba jambo linalomhusu mtu fulani au uzoefu wake ni wa kweli au si wa kweli, na usimbague mtu kwa sababu yoyote kwa msingi wa umri, hali ya ndoa, ulemavu, dini, kabila, tabaka, jinsia, utambulisho wa mnyanyasaji n.k.

| | |
|---|---|
| TOA simu yako au kifaa cha mawasiliano, iwapo unaona ni salama kufanya hivyo, kwa manusura/mhanga kuwasiliana na mtu anayemwamini. | USIJARIBU kuleta amani, kusuluhisha au kutatua hali kati ya mtu aliyepitia GBV na mtu mwingine yeyote (kama vile mnyanyasaji, au mtu mwingine yeyote wa tatu kama vile mwanafamilia, mwanakamati wa kamati ya jamii, kiongozi wa jamii n.k.). |
| OMBA idhini/ridhaa ya manusura/mhanga kabla ya kuchukua hatua yoyote. | USISHIRIKISHE kila kitu cha tukio na vitu vya kumtambulisha manusura/mhanga na yeyote. Hii ni pamoja na wanafamilia ya manusura/mhanga, askari/walinda usalama, viongozi wa jamii, wenzako, wasimamizi, n.k. Kushirikisha jambo hili kunaweza kusababisha madhara zaidi kwa manusura/mhanga. |
| MALIZA mazungumzo kwa njia ya kusaidia. | USIULIZE kuhusu au kuwasiliana na manusura/mhanga baada ya kumaliza mazungumzo.. |

## Mifano ya mambo ya kusema…

- “Mazungumzo yetu yatabaki kati yetu.”
- “Mimi siyo mshauri, hata hivyo, naweza kukupa habari nilizonazo. Kuna baadhi ya watu/mashirika ambayo yanaweza kutoa msaada kwako na/au kwa familia yako. Je, ungependa kuyafahamu?”
- “Hapa kuna kila kitu cha huduma, ikiwa ni pamoja na mahali, saa ambazo huduma inapatikana, gharama (iwapo zinatumika), uchaguzi wa usafiri na jina la mtu ambaye unaweza kuzungumza naye.”
- “Je, kuna yeyote unayemwamini unayeweza kwenda kumwomba msaada, labda mwanafamilia au rafiki? Je, ungependa kutumia simu yangu kumpigia yeyote unamhitaji muda huu?”
- “Inapokuja kwa hatua zinazofuata, unachotaka na unafarijika nacho ndicho cha kuzingatiwa zaidi.”
- “Usijione kushinikizwa kufanya uamuzi wowote sasa. Unaweza kufikiria kuhusu mambo na kubadilisha mawazo baadaye.”
- “Siwezi kuzungumza na yeyote kwa niaba yako ili kujaribu kusuluhisha hali. Lakini ninachoweza kufanya ni kukusaidia wakati wa mazungumzo yetu na kusikiliza uliyo nayo.”
- “Inaelekea una mpango wa jinsi ambavyo ungependa kuendelea kutoka hapa. Hiyo ni hatua nzuri.”

# Naendeleaje hatua kwa hatua?

## Ni miongozo gani ya msaada wa kwanza wa kisaikolojia

## Mtazamo Wa Manusura/ Mhanga

### Faida na hatari za kutafuta msaada


Kutafuta huduma si salama siku zote kwa manusura/mhanga na kunaweza kusababisha madhara zaidi. Kumbuka kwamba wajibu wako ni kutoa habari sahihi, mpya kabisa juu ya huduma zinazopatikana na kumwacha manusura/mhanga afanye uamuzi wake mwenyewe juu ya mambo yanayohusu usalama wake. Zingatia mfano ufuatao wa faida au hatari:

**HATARI za kutafuta msaada**

- Uwezekano kwamba rafiki wa manusura/mhanga, familia na/au jamii itagundua, ambapo jambo hili linaweza kusababisha kunyanyapaliwa, kufukuzwa nyumbani au katika jamii, na/au kufanyiwa ukatili zaidi.
- Uwezekano kwamba mnyanyasaji anatambua kwamba watu wengine wanafahamu kilichotokea, na hali hii husababisha kulipiza kisasi kwa kumdhuru au hata kumuua manusura/mhanga.
- Uwezekano kwamba watoaji huduma wanakuwa katika hatari ya vitisho na ukatili kutoka kwa mnyanyasaji au jamii iwapo anaonekana akimsaidia manusura/mhanga.
- Uwezekano wa majibu ya kutojali, ya kibaguzi, na au yenye hisia za chuki kutoka kwa watoa huduma iwapo hawajafundishwa vizuri.

**FAIDA za kutafuta msaada**

- Upatikanaji wa msaada wa kuokoa maisha wakati una dhiki.
- Upatikanaji wa huduma ya matibabu salama, yanayolinda usiri na ya kitaalamu katika muda ufaao ambao ungeweza kuzuia virusi vya ukimwi na mimba isiyotarajiwa.
- Upatikanaji wa huduma zingine ambazo huongeza hadhi na faraja zaidi, ikiwa ni pamoja na uchaguzi kwa usalama na msaada wa saikolojia ya jamii.
- Upatikanaji wa msaada unaoweza kuzuia ukatili zaidi usitokee.



# Unyanyasaji Na Ukatili Wa Kingono

## Na mdau wa maendeleo/masuala ya kibinadamu au mtu binafsi anayehusika na msaada na huduma




**Ulinzi dhidi ya Unyanyasaji na Ukatili wa Kingono (PSEA)** ni istilahi inayotumika kurejea hatua zilizochukuliwa na wadau wa maendeleo na masuala ya kibinadamu (pia na wafanyakazi wahusika, kama vile washauri waelekezi, wanaojitolea, walinzi, wakandarasi, madereva, wagawaji, machinga n.k) kuwalinda watu walio kwenye hatari ya unyonyaji na unyanyasaji wa kijinsia.

Unyanyasaji na Ukatili wa Kingono (SEA) ni aina ya GVB, kwa vile wahanga wa SEA, mara nyingi wananyanyaswa kijinsia kwa sababu ya kutolindwa kwao, hadhi yao ya mkingamano kama wanawake, wasichana, wavulana, au hata wanaume (katika baadhi ya mazingira). **Ni amri wajibu wa kutoa taarifa za kesi zote za SEA zinazowakilisha tofauti muhimu kati ya makundi hayo mawili (kwa vile GBV haina amri ya wajibu wa kutoa taarifa).**

Wajibu wa kutoa taarifa za SEA unaweza kuibua maswali magumu na changamoto zinazohusiana na ridhaa, ambayo haina budi kuazimiwa kwa uratibu wa karibu na Mratibu wa Wakala wa Ndani wa PSEA. Inapendekezwa kwamba wafanyakazi wote wanaoweza kupokea moja kwa moja taarifa za moja kwa moja za SEA wapate mafunzo juu ya jinsi ya kutoa habari za mipaka ya usiri (kwa maneno mengine, kupata ridhaa inayotokana na ufahamu kamili wa jambo)[3] kabla ya kuwekwa wazi. Hii haitatui kikamilifu masuala ya usiri, ridhaa inayotokana na ufahamu kamili wa jambo, na utoaji taarifa wa lazima, lakini inatoa fursa kwa mlalamikaji/mhanga kutafakari juu ya 'nini' na 'jinsi gani' kabla ya habari kutolewa/kuripotiwa.

Nchini Tanzania, jumuiya ya maendeleo na masuala ya kibinadamu imeahidi kuweka mazingira salama kwa wazee, vijana na watoto wanaoweza kudhuriwa. Kwa hiyo, ni muhimu uzifahamu kanuni:

- SEA haukubaliwi na umepigwa marufuku kwa wafanyakazi wote wa kimataifa na kitaifa (kama wanafanya kazi na Umoja wa Mataifa au wabia wanaotekeleza mradi).

- Ni marufuku kabisa kuwa na mahusiano na yeyote chini ya umri wa miaka 18 (bila kujali umri wa ridhaa mahali au katika nchi ya kuzaliwa).

- Ni marufuku kabisa kuwa na mahusiano na yeyote kwa lengo la kubadilishana vitu, huduma, ajira, na/ au upendeleo. Hii ni pamoja na aina yoyote ya ukahaba (kwenye kituo cha kazi na nchi ya kuzaliwa).

- Ni marufuku kabisa kwa wafanyakazi wote wa Umoja wa Mataifa na wabia kushiriki katika aina yoyote ya tabia ya udhalilishaji wa kijinsia, kushusha hadhi, na/au ya unyonyaji.

Aidha, unapaswa ufahamu kabisa kwamba:

- Kitendo chochote cha SEA kitachunguzwa na hatua za adhabu zitachukuliwa, iwapo kutakuwa na sababu ya kufanya hivyo.

- Kitendo chochote cha SEA kilichothibitishwa kitasababisha hatua kuchukuliwa, ikiwa ni pamoja na siyo tu kusimamishwa kazi, kurudishwa kwao mara moja (kama ni mfanyakazi wa kimataifa), kufukuzwa kazi, na/au kuzuiwa kufanya kazi tena baadaye.

- Una wajibu kutoa taarifa za SEA mara moja kwa njia ya utaratibu wa PSEA (na siyo kuchunguza mwenyewe). Kushindwa kufanya hivi ni uvunjaji wa Kanuni za Maadili Mema.

- Mtu binafsi anayetoa taarifa kwa nia njema ana haki ya kulindwa dhidi ya ulipizaji kisasi, ambapo taarifa za uwongo zenye nia mbaya ni mwenendo mbaya na kinyume cha miiko ya watendaji.

**Hata hivyo, mpango wa utaratibu wa kumsaidia manusura/mhanga yeyote wa SEA unabaki uleule kama ilivyo kwa matukio mengine ya ukatili wa kijinsia (kama ilivyoelezwa humu).**

Malalamiko kuhusiana na SEA nchini Tanzania yanaweza kutolewa taarifa moja kwa moja na mhanga mwenyewe au na yeyote yule anayeweza kuwa na mashaka na/au tatizo, kwa mfano, wafanyakazi, wabia, wanaojitolea, wafadhili, jumuiya zilizoathiriwa, nk. Ni muhimu kwamba yeyote anayeweza kupokea lalamiko kuhusiana na SEA nchini Tanzania ahakikishe:

Kwa majukumu ya ziada yanayotokea wakati kitendo kilichotendeka kinahusiana na unyonyaji na unyanyasaji wa kijinsia, unatakiwa kutafuta msaada na mwongozo kutoka kwa:

- Msimamizi wako/mkuu wa ofisi.

- Mtoa Taarifa za PSEA kutoka kwa ama shirika lako au shirika lingine mwanachama wa Mtandao wa PSEA Tanzania.

- Mratibu wa Wakala wa Ndani wa PSEA au wenyeviti wenza wa Mtandao wa PSEA.

- Omba msaada kupitia tovuti ya PSEA ya Umoja wa Mataifa Tanzania.

[3] Hii inabidi ielezwe katika lugha yao na kwa namna ambayo ni rahisi kwa mlalamikaji/mhanga kufahamu (a) habari na undani wa yale yatakayokuwa yametolewa taarifa, (b) nani atakayepata hizi habari, na (c) ni aina gani za hatua za ufuatiliaji zinazoweza kuchukuliwa. Mlalamikaji/mhanga atasaidiwa na Mtandao wa PSEA kufahamu vizuri zaidi mchakato na kudai haki yake ya usiri.

# Yoyote anayepokea malalamiko ya SEA nchini Tanzania anatakiwa kufanya yafuatayo:



Anajali hadhi na heshima ya mhanga, au mlalamikaji (kama ni tofauti) siku zote akimwamini mhanga, kutunza faragha na kumfanya afarijike kadri iwezekanavyo.

Amweleze mhanga/mlalamikaji hitaji la lazima kutoa taarifa kuhusiana na madai yote ya SEA na kutafuta ridhaa inayotokana na ufahamu kamili wa jambo kutoa habari kwa usiri. Iwapo mhanga hajaridhia kutoa taarifa ya tukio, kuna hata hivyo, wajibu wa kutoa taarifa.






Apate taarifa za msingi za tukio na aulize tu maswali yanayotakiwa ili kupata ufahamu mzuri wa lalamiko la SEA, ili liweze kupelekwa kwa salama kwa wakala anayefaa. Hii inajumuisha kushughulikia nini, wapi, lini na nani.



Apeleke lalamiko la SEA kwa ama Mtoa Taarifa za PSEA wa wakala husika au Mratibu wa Wakala wa Ndani, atakayeendeleza mchakato.

# ANDAA

Maandalizi ni muhimu. Hata bila mtetezi wa kampeni dhidi ya GBV anayepatikana kwenye eneo lako, kunaweza kuwa na huduma zingine, ikiwa ni pamoja na kwa kiwango cha mahali/jamii, ambazo zinaweza kuwa za msaada kushughulikia mahitaji ya mtu. Huenda unafahamu huduma zaidi kuliko unavyofikiria!

## Angalia huduma zinazopatikana

- Tumia Karatasi ya Taarifa (ukurasa wa 5 & 6) kujaza taarifa kuhusu huduma zinazopatikana. Fanya kazi na mtaalamu wa GBV, watoa taarifa za PSEA, kiongozi wa timu yako, wenzako na wabia wengine. Jaza taarifa muhimu kuhusu jinsi ya kupata hizo huduma, ikiwa ni pamoja na wapi pa kwenda, nani wa kuzungumza naye, na ni nani anaweza kuzipata/kutozipata (kwa mfano, wanawake pekee, uandikaji wa hati muhimu, n.k.).
- Muulize mtoa taarifa za PSEA kuhusu itifaki za Kuzuia Unyanyasaji na Ukatili wa Kingono. Ikitokea wakala wako hana itifaki iliyowekwa ya PSEA, nenda kwa Mtandao wa PSEA Tanzania kwa mwongozo katika mazingira yako.

## Mazoezi huleta ufanisi

- Ridhika na miswada ya sampuli kwenye kurasa za 7-10. Fanya mazoezi kwa sauti au na wenzako na marafiki. Kadri unavyofanya mazoezi ndivyo utakavyofarijika zaidi iwapo manusura/mhanga wa GBV anaomba msaada wako.
- Rejea Kitabu cha Vidokezo kwa Mtumiaji kwa habari za ziada juu ya jinsi unavyoweza kujifunza/fanya mazoezi ya nyenzo hizi.
- *Kitabu cha Mwongozo* kinamsaidia yeyote anayepitia hali ngumu. Wakati ujao mwenzako au rafiki akija kwako kutafuta msaada au ushauri, fanya mazoezi kwa kutumia maswali na maelezo yaliyomo humu.

# ANGALIA

Wakati mtu anafunua tukio lake la unyanyasaji wa kijinsia kwako…

## Jitambulishe

- Jitambulishe jina lako, wajibu wako na wewe ni nani. Uliza jinsi unavyoweza kusaidia.

## Shughulikia mahitaji ya msingi na ya haraka

- Kila mtu atakuwa na mahitaji tofauti ya kimsingi, yanayoweza kuwa huduma ya matibabu ya haraka, maji, kumtafuta mpendwa au blanketi au nguo iwapo zilipotea, zimechanika, zina madoadoa au zimeondolewa. Hasa kwa manusura/wahanga wa GBV, nguo zinaweza kuwa ndilo hitaji la msingi na la dharura kwao ili kufarijika na kuwa na hadhi zaidi.
- Mwache manusura/mhanga akwambie jinsi anavyoona kuhusu usalama wake binafsi. Angalia usitegemee mawazo yako kwa yale unayoyaona.

## Angalia njia tofauti watu wanazotumia kutafuta msaada

- Ruhusu watu kuonyesha hisia zao kwa njia yoyote ile wanayotumia. Watu wana namna yao ya kukabiliana na dhiki na shida. Baadhi ya watu wanaweza kunyamaza na kushindwa kuzungumza; kukasirika na kupiga kelele; wakijalaumu kwa yale yaliyotokea kwao; wakilia; wakifanya vurugu na kadhalika.
- Watu wenye ulemavu, watu wanaozungumza lugha tofauti na wengine hupitia vikwazo tofauti wanapotafuta msaada. Shika kanuni zinazomlenga manusura/mhanga na usiri wakati ukitafuta njia za kuwasikiliza na kuwasaidia watu hawa. Hata kama huwezi kumwelewa mtu unaweza siku zote kuonyesha unajali na msaada.
- Hakikisha mfanyakazi mwanamke yupo ili kutoa msaada, hasa katika muktadha ambapo wanawake na/au wasichana kutokana na utamaduni wao hawawezi kuwa na mwingiliano na wanaume.

## Tambua unayoweza na usiyoweza kusimamia

- Kuna hali inayohitaji msaada maalumu zaidi ya wajibu wako, kama vile hali inayowahusisha watoto, kutoa taarifa kwa lazima,[4] hatari ya mara moja kwa manusura/mhanga, au ambapo manusura/mhanga anaweza kujidhuru mwenyewe au kuwadhuru wengine. Wanaweza kuwepo watoa taarifa za PSEA wanaoweza kutoa msaada vizuri zaidi katika hali kama hii. Rejea kwenye Karatasi yako ya Taarifa (ukurasa wa 5 & 6).

## ! KUMBUKA

Iwapo unataka kutafuta msaada kutoka kwa msimamizi au mwenzako mwingine, **SIKU ZOTE omba idhini kutoka kwa manusura/mhanga** kwanza. Mwambie manusura/mhanga mtu unayetaka kuzungumza naye, kwa nini unataka kuzungumza naye na habari gani unataka kumshirikisha kuhusu yeye Iwapo.

[4] Kuna mazingira ambayo yana kanuni za kutoa taarifa kwa lazima kwa aina fulani ya kesi. Rejea kwa mtoa taarifa za PSEA na/au mtaalamu wa GBV kwa habari na mwogozo zaidi.

# SIKILIZA

Baada ya kuhakikisha kwamba mahitaji ya msingi ya manusura/mhanga yametimizwa, na kwamba hayuko katika hatari ya mara moja, SIKILIZA.

Manusura/mhanga anaweza kuvurugwa na/au kuchanganyikiwa, lakini kama msaidizi ni muhimu kuwa na utulivu kadri iwezekanavyo. Mruhusu mtu binafsi kukushirikisha habari nyingi au chache jinsi apendavyo. Si wajibu wako kumshauri, kumpeleka mtu kwenye huduma au kufanya mahojiano ya kina kuhusu jambo lililotokea kwake. Badala yake, sikiliza tu au, kama inahitajika, uliza maswali kama “naweza kukwambia kuhusu huduma ambazo zinapatikana kukusaidia”? Au “ungependa nikusaidieje?”

## ZINGATIA

Ni vizuri zaidi kuepuka maswali hasa yale yanayoanza na “KWA NINI” kwa vile maswali kama hayo yanakuwa kama yanalenga kumlaumu manusura/mhanga. Badala yake, sikiliza tu au, kama inahitajika, uliza maswali kama “naweza kukwambia kuhusu huduma ambazo zinapatikana kukusaidia?” Au “Ungependa nikusaidieje?”

## Nguvu Ya Kusikiliza

Wakati mwingine unaweza kuwa katika hali ambayo hakuna huduma kabisa au rasilimali za kukuwezesha kushirikishana na manusura/mhanga. Unaweza kujiona huna msaada. Ni muhimu kwamba unakuwa mwaminifu kwa manusura/mhanga, ukitambua ujasiri wa kukushirikisha uzoefu wao kwako, onyesha kwamba unasikitika huwezi kuwa tena msaada na onyesha unamheshimu manusura/mhanga kadri iwezekanavyo wakati wa mazungumzo yenu. Kuonyesha kwamba upo na unasikiliza vizuri wenyewe tu ni msaada.

## UNGANISHA

Unavyomsaidia manusura/mhanga kufanya maamuzi kuhusu hatua zake zinazofuata…

### Muulize manusura/mhanga iwapo kuna mtu anayemwamini kwenda kwake kutafuta msaada.

- Iwapo unaulizwa maoni yako ni nini, mtie moyo manusura/mhanga kufanya maamuzi kuhusu ni nani wa kwenda kwake, lini na kwa nini.
- Usitoe maoni yako mwenyewe kuhusu hali.

### Iwapo huduma zipo, toa habari sahihi kwa manusura/mhanga kuhusu huduma zinazopatikana au uchaguzi unaoleta faraja zaidi.

- Maandalizi ni muhimu. Tumia **Karatasi yako ya Taarifa (ukurasa 5&6)** na uhakikishe una habari sahihi, mpya kabisa kuhusu huduma zinazopatikana na jinsi ya kuzipata.
- Iwapo huna hakika kwamba huduma fulani ipo, sema huna hakika.

### Kamilisha mazungumzo kwa huruma.

- Dumisha usiri.
- Imarisha maamuzi yoyote ambayo manusura/mhanga alifanya.
- Kumbuka, wajibu wako ni kumsaidia manusura/mhanga katika uamuzi na uchaguzi wake, hata kama manusura/mhanga hafanyi hivyo. Usishiriki vikao au mikutano inayorudiwa na manusura/mhanga, wala kusimamia kesi ya manusura/mhanga.

## Baada ya mazungumzo

**Kutafakari na kujitunza:** Ni muhimu kukumbuka kwamba unaweza kufanya kila kitu vizuri, lakini huendi kusuluhisha tukio la huyu mtu au kuondoa uchungu wake. Kusikiliza na kusikia uzoefu wa watu wengine kunaweza kukuweka katika hatari ya tukio lao la uchungu, kutia kiwewe au la kuumiza–pia hutambulika kama kupitia katika kiwewe cha mara ya pili. Fikiria jinsi ya kujitunza wakati hisia hizi zinapokuja kwako. Fikia mfumo na mtandao wako wa msaada, kwa ikiwa ni pamoja na wenzako, kiongozi wa timu yako au mtaalamu wa GBV, kuuliza juu ya kubadilishana (ukikumbuka usiri wa manusura/mhanga) na kutafuta msaada.

Kwa vile aina fulani za ukatili (kwa mfano, ukatili wa kifamilia) zinaweza kutokea kwa kujirudiarudia, unaweza kumuona mtu huyu tena au kufahamu kwamba alipitia tukio lingine la ukatili. Huwezi kubadilisha mambo waliyopitia, lakini unaweza:

- Kusikiliza bila ya kuhukumu manusura/ mhanga wakati wa kila tukio bila ya kujali iwapo umezungumza nao awali au la.
- Fikiria jinsi ya kuboresha mpango (wa mfuatano wa mambo ya kutekelezwa) wako, fanya huduma unazotoa kuwa salama zaidi, na weka mazingira chanya zaidi kwa wale wanaopitia GBV.



# Inakuwaje kama muhanga anayenifata ni mtoto au kijana?

# Kuwasaidia watoto na vijana balehe hadi kufikia miaka 18

## Ujumbe muhimu

**Siku zote zungumza na mtaalamu wa kumlinda mtoto dhidi ya GBV katika nchi/muktadha wako kwanza kufahamu:** (1) ni huduma zipi zinazopatikana katika eneo lako na (2) itifaki za mahali na taratibu.[5]

**Usidhuru.** Usiwatafute watoto manusura/wahanga. Siyo kazi yako kuchunguza au kukagua iwapo mtoto/kijana aliyebalehe hadi kufikia umri wa miaka 18 anapitia ukatili. Kufanya hivyo kunaweza kusababisha ukatili zaidi na hatari kwa mtoto/kijana. Kuwa wa kufikiwa iwapo mtoto/kijana anataka kutafuta msaada wako.

**Kumbuka jukumu lako.** Iwapo mtoto/kijana aliyebalehe hadi kufikia umri wa miaka 18 anakuja kukuomba msaada,

(1) Msikilize bila ya kuhukumu.

(2) Msaidie mtoto/kijana kwa kumuunganisha na mtu mzima ambaye mtoto/kijana anamtambua kuwa salama na wa kuaminika. Huyu **anaweza asiwe** mzazi wake, mtunzaji au mwanafamilia.

(3) Usifanye maamuzi kwa ajili yake, ikiwa ni pamoja na kumlazimisha mtunza mtoto/kijana au mtu mwingine yeyote kuwa naye wakati anazungumza nawe.



**! KUMBUKA,** iwapo mtetezi wa kampeni dhidi ya GBV au wa ulinzi wa mtoto anapatikana katika eneo lako, wezesha rufaa salama na ya siri ya mtoto/kijana kwa mtaalamu ili kumsaidia vizuri zaidi.

Tumia mwongozo huu tu iwapo **hakuna mtetezi wa kampeni dhidi ya GBV au wa ulinzi wa mtoto aliye katika eneo lako.**

**Toa faraja.** Mruhusu mtoto/kijana kuongoza mazungumzo, hata kama hii inamaanisha kuwa naye katika ukimya. Mwangalie machoni na angalia lugha ya mwili ya wazi kumwonyesha mtoto/kijana kwamba anaweza kujifunua kwako iwapo anataka. Usiulize maswali kuhusu yaliyotokea,

[5] Rejea watalaamu wako wa ukatili wa kijinsia GBV au ukatili dhidi ya watoto (VAC) nchini kuhusu itifaki za ndani na taratibu, ikiwa ni pamoja na: (1) mipaka ya usiri na (2) utawala wa sharia, na (3) watoa taariza za PSEA.

na nani na kwa nini – badala yake tumia maelezo na zungumza kwa namna anayoweza kufahamu.

**Mfanyie kila mtoto kwa usawa.** Watoto wote hawana budi kupewa msaada sawa bila ya ubaguzi kwa msingi wa jinsia yao, umri, hali ya familia, hali ya watunzaji wake au sehemu nyingine yoyote ya utambulisho wao. Usimfanyie mtoto ambaye amepitia GBV kama asiyekuwa na msaada. Kila mtoto ana uwezo wa pekee na nguvu na ana uwezo wa kupona. Zungumza na mtoto manusura/mhanga kwa namna anayoweza kufahamu na kwa kuheshimu hadhi na maoni yao.

**Dumisha usiri.** Usiandike, usipige picha, au kuweka katika nyaraka kwa njia yoyote ile mwingiliano wako na mtoto/kijana. Weka mbali simu zozote au kompyuta ambazo zinaweza kuonekana kwamba zinarekodi mazungumzo. Omba idhini kumshirikisha kuhusu mtoto/kijana au uzoefu wao. Hii inamaanisha iwapo kuuliza iwapo unaweza kumshirikisha habari mtu mwingine ambaye mtoto/kijana anamtambua kama mtu mwaminifu.

**Hakikisha usalama wa mtoto.** Usalama wa kimwili na wa kihisia wa mtoto ndilo jambo la msingi. Zingatia usalama wa mtoto katika miingiliano yote naye, na kwa kuhusiana na hatua zozote zinazochukuliwa.

Katika baadhi ya matukio inaweza isiwe wazi kusaidia kukosa kufahamu jinsi ya kusaidia **mapendeleo bora ya mtoto** na maslahi yake ya kimwili na kiakili. Iwapo huna hakika ya usalama wa hali, mfahamishe mtoto kwamba utahitaji kuzungumza na mtoaji mwingine wa huduma kwa siri au mwanatimu ambaye anaweza kuwa na ufahamu zaidi jinsi ya kuhakikisha usalama wake.[4]

**Angalia jinsi mtoto/kijana au mtunzaji wao anaweza kutafuta msaada.** Watoto na vijana hutafuta msaada katika njia tofauti kuliko watu wazima, na ni mara chache sana wanaweza kusema waliyonayo moja kwa moja. Watoto wanaweza kuwa na ugumu wa kumwamini au kuzungumza na watu wazima, hasa watu wazima wasiowafahamu vizuri; huogopa, kudhalilishwa au kuaibika; au kuogopa kuonyesha hisia zao. Unaweza: (1) kusikia uvumi wa udhalilishaji wa mtoto, (2) kufikiwa na watu wazima wakitafuta msaada wa mtoto au (3) hisi udhalilishaji wa mtoto, kutokana na ishara au tabia ya mtoto.

## Ikiwa mtu anakuuliza msaada kumhusu mtoto/kijana aliye na hitaji…

| Mambo Ya Kufanya | Mambo Ya Kutofanya |
|---|---|
| TOA habari sahihi na mpya kabisa kuhusu huduma zinazopatikana kwa mtu aliyekuuliza kusaidiwa. | USICHUNGUZE uvumi au kutafuta kumpata/kumhoji mtoto/kijana. |
| HESHIMU usiri.[4] | USIJADILI au kushirikisha kila kitu unachokifahamu kutoka kwa mtu yeyote.[4] |

## Ikiwa mtoto/kijana anakuomba msaada…

### ANGALIA



| Mambo Ya Kufanya | Mambo Ya Kutofanya |
|---|---|
| MUULIZE mtoto/kijana iwapo anataka kupata mahali palipotulia na pa siri ili kuzungumza. Hakikisha ni mahali ambapo wengine wanaweza kukuona, lakini hawawezi kukusikia. | USIMUELEKEZE mtoto/kijana kwenda mahali palipotulia sana au pa siri, au kumtenga mtoto dhidi ya mapenzi yake. |
| HAKIKISHA kwamba unakaa kwa namna unayoweza kumwangalia machoni. Dumisha lugha ya mwili ya wazi. | USIMGUSE, kumkumbatia au kumshika mwilini kwa kuwa jambo hili linaweza kuleta kiwewe, kukosesha raha na la kusumbua. |
| WAULIZE wasichana na wavulana iwapo wanataka kuzungumza na mtu mzima mwanamke au mwanaume wa jinsia moja na wao. | |

# SIKILIZA



## Mambo Ya Kufanya

SIKILIZA kwa umakini na uwe mwangalifu kwa mawasiliano ya mwili yasiyotumia maneno.

KUWA mtulivu na mwenye subira, kwa kukubali yanayosemwa bila ya kuhukumu.

MUACHE mtoto/kijana ajieleze kwa kutumia maneno yake.


## Mambo Ya Kutofanya

USIFANYE mahojiano au kukadiria. Usiandike kitu, usipige picha au kumshirikisha mtu habari kuhusu mtoto/kijana au uzoefu wao.[4]

USIONYESHE mshtuko, hali ya kutoamini, hasira au kufanya jambo lolote linalosababisha shida kwa mtoto/kijana.

USITUMIE maneno makubwa au kusema zaidi ya mtoto/kijana.

# FARIJI



## Mambo Ya Kufanya

MHAKIKISHIE mtoto/kijana kwamba ni SAWA yeye kukueleza kilichotokea.

HESHIMU maoni, imani na mawazo ya mtoto.

TUMIA maneno ya kufariji yanayofaa katika muktadha wa utamaduni… mifano ni pamoja na:

“Nakuamini” – jenga imani

“Nafurahi kwamba uliniambia” – hujenga uhusiano na mtoto

“Asante kwa kunishirikisha uzoefu wako” – huonyesha maono ya kuhisi maono ya mwingine

“Wewe ni jasiri sana kuzungumza nami” – kumhakikishia na kumuimarisha

## Mambo Ya Kutofanya

USIAHIDI usiyoweza kutimiza kama vile kusema “kila kitu kitakuwa SAWA” wakati jambo lenyewe halipo kwenye uwezo wako kumhakikishia mtoto ustawi wake.

USIMLAZIMISHE mtoto/kijana kuendelea kuzungumza nawe iwapo hataki.

# UNGANISHA

## Mambo Ya Kufanya

ULIZA iwapo kuna mtu ambaye mtoto/kijana anamwamini, na iwapo anahitaji msaada umufikie mtu huyo, au kuambatana naye ili kumtafuta mtu huyo.

KAA na mtoto/kijana mpaka ajisikie salama au katika uangalizi wa mtu anayemwona ni salama na wa kuaminika.

MWAMBIE mtoto/kijana na mtu mzima anayemwamini kuhusu huduma zinazopatikana na jinsi ya kuzipata.

SEMA unachokifahamu. Sema “sijui” au “sina hiyo habari” iwapo huna habari iliyoombwa.

## Mambo Ya Kutofanya

USIMLAZIMISHE mtoto/kijana kuwa na mtunzaji wake au mtu mwingine yeyote wakati anapozungumza nawe kwa sababu watu hawa wanaweza kuwa ndio wao waliofanya unyanyasaji, au mtoto/kijana anaweza asitake kuwashirikisha aliyonayo.


USIMWACHE mtoto/kijana peke yake akiwa katika shida (kwa mfano, kulia, kukasirika au kushtuka).

USIJARIBU kutatua tatizo mwenyewe, fanya mpango au kufanya maamuzi kwa ajili ya mtoto/kijana.

# Marejeo kwa umri na uwezo wa watoto kufanya maamuzi

Fahamu kwamba mtaalamu mtendaji – aliye na uzoefu wa kufanya kazi na watoto/vijana wanaopitia GBV – yupo katika nafasi nzuri kabisa kutambua uwezo wa mtoto/kijana wa kufanya maamuzi kwa kushirikiana na mtoto/kijana mwenyewe na mtunzaji wake.

**Wajibu wako kama mtu asiyekuwa mtaalamu ni kusikiliza na kumfariji mtoto/kijana, kumuunganisha kwa mtu anayemwamini, na kushirikisha habari kuhusu huduma zinazopatikana.** Makundi ya umri wa makundi yaliyo ainishwa hapa chini ni kwa ajili ya kufanya marejeo tu na yanaweza kubadilika kulingana na umri, kiwango cha ukomavu, kiwango cha maendeleo na mambo mengine.



**Vijana wakubwa wa umri wa miaka 15 na zaidi** kwa jumla ni wakomavu wa kutosha kufanya maamuzi yao wenyewe na kufahamu mambo wanayoyapitia.

**Wajibu wako:** (1) msikilize kijana anaposhirikisha mambo anayoyapitia, (2) msaidie kijana kuungana na mtu anayemwamini kwa ajili ya msaada unaoendelea na (3) toa habari kuhusu huduma zinazopatikana na jinsi ya kuzipata.



**Watoto wadogo miaka 6 hadi 9 na vijana wa miaka 10 hadi 14** wanaweza au hawawezi kueleza wenyewe ukatili walioupitia. Wanaweza au hawawezi kufanya maamuzi peke yao.

**Wajibu wako:** (1) msaidie mtoto/kijana kumpata mtu mzima anayemwamini kumsaidia katika hatua zinazofuata na (2) kutoa habari kuhusu huduma zinazopatikana na jinsi ya kuzipata na mtoto/kijana na mtu mzima aliyetambuliwa.



**Watoto wachanga wa miaka 0 hadi 5** hawatatoa taarifa ya ukatili kwa sababu ya ukosefu ya kukosa au kuwa na uwezo mdogo wa mawasiliano. Mtu mwingine (kama vile rafiki, mtunzaji, mwanafamilia, mwanajamii n.k) ataomba msaada kwa niaba ya mtoto.

**Jukumu lako:** toa habari kwa mtu aliyeambatana na mtoto kuhusu huduma zinazopatikana na jinsi ya kuzipata.

*Yametoholewa kutoka: UNHCR, Mwongozo wa Uamuzi wa Uamuzi Bora, 2008. IRC/UNICEF, Kwa Kuwatunza Watoto Manusura wa Ukatili  wa Kijinsia, 2012.*



**Kitabu hiki ni Mwongozo unaoendana na miongozo ya IASC GBV ya mwaka 2015.**

www.gbvguidelines.org

Ikoni za Google Play na iTunes – Kitabu cha Mwongozo wa GBV